MAOMBI

Ya Kujikuza kiroho

SEHEMU YA 1

BY DENIS & DEVIS JULIUS

MAOMBI MAALUMU YA KUJIKUZA KIROHO.

Sehemu ya 1

UTANGULIZI:

Nakusalimu katika jina la mwokozi wetu Yesu Kristo.

Huu ni mfufulizo wa maombi maalumu katika eneo la "***ukuaji kiroho***". Kila mmoja wetu aliyeokoka, anao wajibu wa kuhakikisha anakua kiroho. Na ukuaji wa kiroho hutegemea mambo mawili makubwa,

1. **NENO LA MUNGU.**
2. **MAOMBI**

Kama mtakatifu ulieyokoka, ni wajibu wako kusoma na kutafakari mwenyewe biblia, lakini pia na "kufundishwa". Hivyo huna budi kufanya mambo hayo kila siku, na kwa jinsi unavyoingiza sana maarifa ya Neno la Mungu ndivyo ukuaji wako wa kiroho nao unavyoongezeka kwa kasi. Ikiwa utapenda kupata mafundisho ya Neno la Mungu, na mistari mingi ya biblia iliyochambuliwa basi Tembelea tovuti yetu hii www.wingulamashahidi.org. Utakutana nayo zaidi ya Elfu nne (4,000). Na kwa sehemu kubwa utapiga hatua kiroho.

Lakini pia, Eneo la **Maombi,** ni muhimu sana. Yaani "Neno na Maombi" vinavyokwenda pamoja, ni kama mbawa mbili za ndege, kamwe hawezi kupaa ikiwa baya moja ni bovu, haijalishi lile lingine litakuwa ni zima kiasi gani.

Lakini kwa bahati mbaya, wengi hawana uelewa wa vipengele vya maombi ambavyo wanapaswa waviombee, ili wakue kiroho. Mwisho wa siku wanaishia kuomba tu waonavyo, utaona wengine wanaomba Bwana awafanikishe mipango yao, awape afya, awatetee katika biashara zao, n.k. Ndugu hayo sio maombi yatakayokukuza kiroho (umekosa shabaha). Huna budi kupata mwongozo sahihi utakaokusaidia kupiga hatua kiroho.

Tutakuwa na mfululizo huo, kila wiki. Na Katika maombi yako ya kila siku ukiongezea na vipengele hivi katika kuomba itakusaidia sana, kujiongeza kiroho.

~Mwl Denis & Devis Julius

TAMANIO LA BWANA (HERI ZA BWANA). (Mathayo 5:1-12)

Tambua kuwa masomo ya kwanza kabisa ambayo Bwana Yesu alianza kuyafundisha hapa duniani. Yalihusu “tamaa” yake kwa watu wote. Yaani tabia ambazo alitamani kila mtu angekuwa nazo hapa duniani. Na ndio hapo akatumia “HERI, HERI, HERI”. Yaani kwa lugha nyingine ni sawa na Yesu aseme, “I wish every one could have these things inside”

Kulikuwa na sababu kwanini aliyafanya hayo kuwa ni fundisho la kwanza, alikuwa anajua umuhimu wake, kwa kila mwanafunzi,. Embu tusome sasa, na kupitia hapo ndipo tutakapotolea vipengele vyetu vya maombi maalumu ya ukuaji kiroho, katika sehemu hii ya kwanza.

> ***Mathayo 5:1*** *Naye alipowaona makutano, alipanda mlimani; na alipokwisha kuketi, wanafunzi wake walimjia; 2 akafumbua kinywa chake, akawafundisha, akisema, 3 Heri walio maskini wa roho; Maana ufalme wa mbinguni ni wao. 4 Heri wenye huzuni; Maana hao watafarijika. 5 Heri wenye upole; Maana hao watairithi nchi.6 Heri wenye njaa na kiu ya haki; Maana hao watashibishwa. 7 Heri wenye rehema; Maana hao watapata rehema. 8 Heri wenye moyo safi; Maana hao watamwona Mungu. 9 Heri wapatanishi; Maana hao wataitwa wana wa Mungu. 10 Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; Maana ufalme wa mbinguni ni wao. 11 Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. 12 Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu*

<u>Vipo vipengele 9, hapo ambavyo vina HERI.</u>

1. Walio Maskini wa kiroho
2. Wenye huzuni
3. Wenye upole
4. Wenye kiu na njaa ya haki
5. Wenye rehema
6. Wenye moyo safi
7. Wapatanishi
8. Wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki
9. Wenye kushutumiwa kwa ajili ya Kristo

Haya ni mambo 9, ambayo Yesu aliona yakiumbika ndani ya mtu yeyote , basi anageuka na kuwa “MBARIKIWA”. Hivyo na sisi, kwa kulijua hili tutaweka nguvu zetu nyingi kuomba juu ya mambo hayo.

Sasa ni vizuri ukatenga walau **<u>dakika 40,</u>** kuomba kwa kuzama, juu ya kila kipengele. Yaani kwa wiki ukaomba kwa **<u>SAA SITA.</u>** Utakuwa umemaliza vipengele hivi vyote 9. lakini kama ukiomba zaidi ya hapo, ni bora. Kumbuka hakuna ukuaji usiokuwa na gharama. Huombi, hupokei. Usipojijenga nafsi mwenyewe, shetani atakusaidia kuijenga kwake. Kataa uvuvi wa kuomba. Shindana na mwili.

MWONGOZO:

1) MASKINI WA ROHONI: (dk 40)

Anafanana na maskini wa kimwili. Ni mtu ambaye hajaridhika kiroho anajiona kama hana chochote, anajiona kama bado hajajijengea daraja lolote kwa Mungu, bado hajamjua Mungu. Na hivyo mtu akiwa hivyo maana yake ni kuwa kila siku atatamani kupiga hatua nyingine kiroho, ili awe tajiri.

Lakini si wakristo wote wenye roho hii, maana kama ingekuwepo kwa wote, kila wakati ungeona watu wanahangaika huku na huko, kumjua Mungu na kumtumikia yeye, na kuutafuta uso wake, kutulia muda mrefu uweponi mwake kusikiliza Neno lake, na kukesha kuomba. Hivyo mwombe Mungu sana eneo hili akujalie ujione maskini. Sifa moja wapo ya mtu aliyekuwa kiroho, huwa kila siku anajiona ndio kwanza ameokoka leo. Anatamani akue zaidi na zaidi. Huyo ndiye maskini wa rohoni. Omba Bwana aufanye moyo wako uwe hivyo.

Tumia dakika zote arobaini (Au zaidi), kumsihi Bwana, akupe kujiona wewe ni maskini wa roho. Na ni hakika, jambo hilo litaumbika ndani yako, kwa jinsi siku zitakavyokuwa zinakwenda.

- Mitume walikuwa ni maskini wa kiroho; Ndio maana walikuwa radhi kumfuata Yesu popote alipokwenda.
- Makahaba walikuwa maskini wa roho, Na hivyo ikiwafanya wanyenyekee kusikiliza mahubiri ya Yohana na ya Bwana, matokeo yake, wakawa wa kwanza kuingia katika ufalme wa mbinguni zaidi ya mafarisayo na waandishi. (Mathayo 21:31).
- Yule mtoza ushuru, alipofika hekaluni kuomba, alijiona alivyo maskini rohoni mbele za Bwana, hivyo alijipiga kifua chake akisimama mbali akiomba rehema, na hivyo akahesabiwa kuwa ana haki kuliko Yule Farisayo aliyejiona yeye ni mkamilifu mbele za Mungu. Hana haja ya kuhudumiwa na yeye (Luka 18:13).
- Watu wa Beroya waliutambua umaskini wao rohoni. Na hivyo walipoletewa habari mpya za neema ya Yesu, hawakupinga moja kwa moja, kama walivyofanya wayahudi wengine. Bali walikaa chini na kuyachunguza maandiko, na hivyo Bwana akawafungua macho yao kuona Yesu Kristo ndio njia ya kweli na uzima.(Matendo 17:10-15).
- Mtume Paulo ijapokuwa alipewa mafunuo mengi namna ile, lakini bado hakujiona amefika. Mpaka anafikia uzee, anamwagiza Timotheo amletee vile vitabu vyake vya ngozi ili avisome (2Timotheo 4:13).

Umaskini wa rohoni, ukiumbika ndani yako .

- ✓ Kiu ya kusoma biblia mda mrefu itaongeza:
- ✓ Kiu ya kuomba itaaamka ndani yako
- ✓ Hofu ya maneno ya Mungu, itaumbika kwa kasi: Hutayachukulia juu juu tu maneno ya Mungu.

Na matokeo yake utakuwa kiroho bila kukwama-kwama!

2. WENYE HUZUNI: (dk 40)

Huzuni sio huzuni ya kidunia itokanayo na mateso ya kiulimwengu, hapana. Bali huzuni ya ki-Mungu juu ya dhambi au makosa. Mtu anayehuzunishwa na dhambi, huwa anatabia ya kumtafuta muumba wake, ili atatuliwe matatizo yake. Na ndio hapo anakutana na neema ya Mungu, ya kusamehewa dhambi na hivyo anafarijiwa. Tofauti na Yule ambaye anapotenda dhambi, hakuna kuugua kokote ndani yake, huwa hana haja na Mungu.

Vilevile, tunapokuwa na huzuni kwa ajili ya dhambi za wengine, na za ulimwengu, tunapoona matendo mabaya, na maovu yanavyotendeka na kuhuzunika tuna heri. Kwasababu hiyo itatupelekea kuwaombea na kuwahubiria, na hatimaye wengi, wanaokoka..

- ✓ Yesu alihubiri kwa nguvu injili ya wazi, yenye maonyo, kwasababu ya huzuni iliyokuwa moyoni mwake kwa ajili yao kwa kutokuamini. (Marko 3:5).

Hivyo na wewe ukiwa na maombi haya. Yakuomba Bwana ayamimine machozi mengi moyoni mwako. Itakupelekea uwe imara sana rohoni. Kwasababu itasukuma, kwanza wewe ukamilishwe, lakini pia uiangaze NURU YA KRISTO Kwa bidii kwa wengine. Ukame na ugumu mioyoni mwetu ndio inayotufanya tuwe baridi, tuvimiliane na dhambi.

Tumia muda mwingi kuombea eneo hili kwa dakika zote 40,. Usiridhishwe na hali yoyote ya dhambi. Bwana aiumbe huzuni yake ndani yako. Augue kwa nguvu ndani,ili ikusukume kushindana na dhambi.

3. WENYE UPOLE: (dk 40)

Upole ni hatua kubwa sana kiroho ambayo tunapaswa tuifikie. Upole sio “mtu kuwa dhaifu”. Hapana, “upole ni ile hali ya mtu kuwa na uwezo, lakini hatumii uwezo wake, kuleta madhara”. Mfano pale Simba anapokuwa na uwezo wa kurarua, lakini hafanyi hivyo, hapo tunasema ni mpole. Lakini sisimizi kwa kuwa hana nguvu ya kurarua mtu, hatuwezi kusema anao upole, kwasababu hatujui kama angepewa nguvu kama za simba, angekuwa vile.

Vivyo hivyo na sisi, Bwana anatamani tuwe na UPOLE, kama aliokuwa nao yeye. Ambapo alikubali kudhihakiwa, kutukunwa, kutemewa mate, kuchapwa mijeledi lakini hakurudisha baya kwa baya, bali aliwaombea msamaha japokuwa alikuwa na uwezo wa kushusha moto ya kuwateketeza.

Kigezo kimojawapo cha mtu kuwa karibu sana na Mungu ni Upole. Musa alikuwa hivyo na ndio maana hatushangai kwanini alimkaribia sana Mungu kwa viwango vile, zaidi ya mtu yeyote duniani (Hesabu 12:3)

Halikadhalika na sisi hatuna budi kuombea jambo hili, ili liumbike ndani yetu. Tuwe watu wa kuachilia, wasiodhuru, wa kusamehe, wala wasiorudisha baya kwa baya.

Omba Mungu akujengee upole. Omba sana kwasababu ni zao la ukomavu wa kiroho..Tumia dakika nyingi, msihi Bwana akuumbie jambo hili.

4. WENYE KIU NA NJAA YA HAKI: (dk 40)

Maana yake Kupenda matendo mema, kupenda kuwa mkamilifu, kupenda haki. Danieli alikuwa ni mtu ambaye hakutaka rushwa, na hivyo mbingu ikampenda, hata hatushangai kwanini alifunuliwa maono makubwa namna ile, ni kwasababu rohoni alionekana ni mkomavu sana. (Danieli 6:4), Ndivyo ilivyokuwa kwa Yusufu kwa ndugu zake. Ndivyo ilivyokuwa kwa Ayubu, aliyependa ukamilifu Bwana akamtokea mwishoni, ndivyo ilivyokuwa kwa Kornelio, Na Anania, na Simoni. Wote hawa walimwona Mungu, kwasababu mioyoni mwao walitamani sana kuwa watu wa HAKI. Si waasi wa sheria za Mungu.

Hivyo na sisi tunapaswa tuombee eneo hili, ili kiu hiyo na njaa hiyo iumbike mioyoni mwetu. Tujione ni wazito katika kufanya maasi lakini wepesi katika kupenda mema na haki.. Furaha yetu iwe ni katika kumcha Bwana.

Omba mwambie Bwana aumbe kiu hiyo ndani yako, kwasababu si wote wanayo. Ikiumbika una heri kwasababu utajazwa.

- ✓ Omba usimamie haki katika ngazi ya kifamilia
- ✓ Kijamii
- ✓ Kazini, masomoni
- ✓ Kanisani

5. WENYE REHEMA: (dk 40)

Rehema ni kitendo cha kughahiri mabaya au adhabu juu ya mtu, hata pale asipokuomba msamaha. Mungu wetu ndivyo alivyo. Anaterehemu kila siku. Na hivyo anatarajia na tabia hii iwe ndani ya watu wake wote, Kuwarehemu wengine. Kuwasemehe, hata pasipo kuomba msamaha.

Tunapokuwa na wingi wa rehema ndivyo na sisi tunavyopokea wingi wa rehema kwa Mungu na hivyo tunapokea vibali vingi, vitakavyojenga mahusiano yetu sisi na yeye.

Omba Mungu akupe moyo huu: wa kuachilia, wa kusamehe,wa kutohesabu mabaya, wa kupenda maadui, wa kutokubeba mambo moyoni. Kumbuka vitu vingi vinazuliwa kwetu kwasababu ya kukosa moyo wa rehema.

Shughulika na hapa kwenye maombi yako, zama, kwa dakika zote 40, ombea Bwana akupe moyo huu.

6. WENYE MOYO SAFI: (dk 40)

Moyo safi, ni moyo usio na uchafu,.

Mambo kama Tamaa za mwili, uasherati, mawazo mabaya, matusi, wizi, hasira, ugomvi, mashindano, uchawi, ibada za sanamu, ulafi Bwana Yesu alisema hutoka moyoni na ndio huuchafua moyo(Soma Marko 7:18-23). Hivyo wewe kama mwana wa Mungu, huna budi kuomba Bwana akupe “Akili” ya kuulinda moyo wako, kwasababu huko ndiko zitokako chemchemi za maji ya uzima.

- ✓ Ombea sana moyo wako. Uwe safi, uwe na uadui mkubwa na mambo machafu. Bwana akupe hamu ya kuupenda usafi wa moyo. Akupe kujiwekea ulinzi, kutoruhusu mambo machafu kukuingia wewe kirahisi moyoni mwako.

Ni eneo muhimu sana ambalo ukifanikiwa basi, thawabu yake ni kuwa utamwona Mungu. Yaani Mungu atajifunua kwako.

7. WAPATANISHI: (dk 40)

Moyo wa upatanishi, ni moyo wa Mungu. Kilichomtoa Bwana Yesu mbinguni kushuka duniani, ni kwa kusudi la kutupatanisha sisi na Mungu. Hivyo na yeye akatuwekea Neno na huduma hiyo hiyo moyoni mwetu (2Wakorintho 5:19). Ili na sisi tuupatanishe ulimwengu kwa Kristo, kwa ile injili tuliyopewa.

- ✓ Hivyo mwombe Bwana afufue kwa nguvu huduma hii ndani yako. Ili ufanane na Kristo. Uwe tayari kuyatoa hata maisha yako kwa ajili ya ukombozi wa wengine, kuwarejesha kwa Mungu. Kumbua Walio na huduma hii mioyoni mwao, kiroho ni watu walio ngazi ya juu sana kwa Mungu, ndio hao wanaojitaabisha wakati wote, kuhubiri injili na kuwapa wengine chakula cha kiroho. Kwasababu huduma hii tayari imeshawekwa mioyoni mwao.

Mlilie Bwana, aiongoze kiu hii. Ili uhamasike kuwahubiri wengine habari njema.

8. WENYE KUUDHIWA KWA AJILI YA HAKI: (dk 40)

Bwana anatamani sote tuwe watu wa “kuitetea haki” kwa gharama zozote, kiasi cha kufikia hatua ya ya hata kuudhiwa kwa ajili ya hiyo.

- ✓ Omba Bwana akupe kuisimamia haki kwa nguvu zote. Bila kutetereka, au kutishwa na mtu au mazingira yoyote. Danieli, aliitetea haki, kwa kukataa kula rushwa hata sheria ilipotoka hakuna kuabudu akaikaidi, akatupwa kwenye tundu la simba. Sasa moyo kama huo wa ujasiri Bwana anataka sote tuwe nao, tunapokusudia kuisimamia haki.

Mwombe, Bwana akupe ujasiri huo.

9. KUSHUTUMIWA KWA AJILI YA KRISTO. (dk 40)

Hapo Bwana anatuonesha kuwa tuwe na moyo wa “kumkiri yeye” bila woga wala haya ya wanadamu. Hata tukifikia hatua ya kushutumiwa, kupigwa, kuchekwa, kuudhiwa kwa ajili yake yake, hatutamsaliti. Wakati mwingine tunaona haya, kwasababu ya ndugu, wazazi, marafiki, jamii, watatuonaje n.k. Lakini Yesu hataki tuwe hivyo, kinyume chake, anapenda moyo wa KUMKIRI yeye, mahali popote. Tusiwe wakristo waoga.

- ✓ Hivyo hapo hatuna budi kumuomba ujasiri, wa kulikiri jina lake, mbele ya familia, jamii, wafanyakazi n.k. Kama ilivyokuwa kwa mitume wake. Tufanyike mashahidi kwelikweli wa Kristo Yesu duniani.

Kwa kuzingatia vipengele hivyo. Ukiombea mambo hayo kwa wiki nzima. Ni hatua kubwa sana, utapigishwa na Bwana, kwasababu umeomba sawasawa na mapenzi ya Mungu. Na kidogo kidogo utakuwa unaongezeka kiroho. Hata kuufikia ukamilifu wa mwaminio.

Usikose mwongozo mwingine wa wiki ijayo..

Bwana akubariki.

Na, Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312